1410/206
KISWAHILI
Oct./Nov. 2019
Muda: Saa 3

HEAD OF DEPARTMENT
LIBERAL STUDIES
SIAYA INSTITUTE OF TECHNOLOGY
P.O. BOX 1087-40600, SIAYA

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# NATIONAL CERTIFICATE IN SOCIAL DEVELOPMENT

KISWAHILI

Saa 3

## MAAGIZO KWA WATAHINIWA

*Mtihani huu una sehemu NNE muhimu:*
***insha, ufahamu, matumizi ya lugha na mbinu na vifaa vya kufundisha.***
*Jibu maswali yote kwenye kijitabu ulichopewa.*
*Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.*
***Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

easytvet.com

HEAD OF DEPARTMENT
LIBERAL STUDIES
SIAYA INSTITUTE OF TECHNOLOGY
P.O. BOX 1087-40600, SIAYA

**Kijitabu hiki kina kurasa 6 zilizopigwa chapa.**

**Watahini ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

© 2019 The Kenya National Examinations Council

**Geuza ukurasa**

## SEHEMU YA KWANZA: INSHA (alama 20)

*Jibu swali moja kutoka sehemu hii.*

1. Andika insha isiyopungua kurasa mbili wala kuzidi kurasa mbili na nusu juu ya mojawapo ya vichwa vifuatavyo:

   (a) Utumizi wa madawa ya kulevya umekithiri nchini. Wewe kama mkurugenzi wa shirika la kumpambana na vileo, andika hotuba utakayoisoma katika mkutano wa hadhara kuhusu madhara ya madawa ya kulevya.

   (b) Akufukuzaye hakwambii toka.

   (c) 'Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana'. Jadili.

   (d) Umaskini umeendelea kusambaa sana katika jamii zetu. Andika insha kuhusu jinsi ya kupambana na umaskini nchini.

   (e) Andika mazungumzo kati ya Mwanasiasa na Mwananchi akimshawishi kwa sababu kemkem kwa nini amchague yeye.

easyelimu.com

## SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (alama 30)

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

2. *Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.*

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru, bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu, kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa siku nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi ilimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanaume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima wa malezi kuwa chombo cha kumtumikia mwanamume, kumstarehesha, kumfariji, kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Democrasia ya jadi naihusudu sana, ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya jiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke aliyeshirikishwa hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya ushiri na uganga. Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa wa uchawi, ulozi na ushirikina. Kwa hivyo wanawake ndio waliokuwa washirikina wakubwa, maana fursa

ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara alipuuzwa na pengine kutukanwa hadharani.

Kwa bahati nzuri kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya. Vita vya wanawake vya kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia.

Wanawake wengi wamekiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kumyanyasa na kumuumbua mwanamke tangu jadi. Watetezi wa haki za wanawake zamani walilaumu suala la serikali za mataifa kutochukua hatua za utekelezaji wa maazimio yaliyoendelea kupitishwa na umoja wa mataifa mwaka had mwaka. Huku masuala ya wanawake ya kijamii, utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa, watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nchi moja. Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengi yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake, kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa, majukumu yao katika jamii, mfuko wa umoja wa mataifa wa wanawake (UNIFEM) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya umoja wa mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu. Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na watu wengine. Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kuukubali ukweli huu; wapende wasipende.

easytvet.com

Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake. Kwa bahati mbaya, itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja na ya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi, wapinga mila na watovu wa utii.

HEAD OF DEPARTMENT
LIBERAL STUDIES
SIAYA INSTITUTE OF TECHNOLOGY
P.O. BOX 1831 - 40600, SIAYA

**MASWALI**

(a) Andika kichwa kinachofaa habari hii. (alama 2)

(b) Eleza chanzo cha dhuluma kwa wanawake. (alama 2)

(c) Huku ukitoa mifano, fafanua hali ya dhuluma kwa wanawake kama inavyodhihirika katika makala. (alama 8)

(d) Eleza hatua ambazo mwanamke amechukua kujikomboa. (alama 4)

(e) Je, jamii imechangia vipi katika kumdunisha mwanamke? (alama 4)

(f) Ni vipi democrasia ya jadi ilivyochangia katika kumdunisha mwanamke? (alama 4)

(g) Fafanua maana ya misemo ifuatayo. (alama 6)

(i) wamekiuka misingi;

(ii) kupitishwa kwa maazimio;

(iii) wanaojitolea mhanga.

## SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (alama 30)

*Jibu maswali yote katika sehemu hii.*

3. (a) Kwa kutungia sentensi, tofautisha vitate hivi. (alama 4)

(i) ghali;

(ii) gari.

easytvet.com

(b) Andika sentensi hii katika wingi. (alama 2)

Chakula chote kimeliwa na maharamia.

(c) Tumia vitenzi vifuatavyo kuonyesha kauli. (alama 4)

| Kitenzi | Kauli | | |
|---|---|---|---|
| | Kutendua | Kutendama | Kutendesha |
| Cheza | ______ | ______ | Chezesha |
| ______ | Kosoa | ______ | ______ |
| ______ | ______ | Ungama | ______ |

(d) Kanusha sentensi hii. (alama 2)

Askari wangalifika mapema wangalimuokoa.

(e) Tumia 'o' rejeshi katika sentensi hii. (alama 2)

Msichana ambaye huja ni mwanasheria.

(f) Kamilisha semi hizi. (alama 4)

(i) Mrefu kama ngamia.

(ii) Simba mwenda pole hajikwai.

(iii) tangaa urembo ya nyota.

(iv) Biwi la maji.

(g) Andika sentensi hii kwa hali ya udogo wingi. (alama 3)

Mtoto amefunga mlango wa nyumba yao.

(h) Tofautisha maana katika sentensi hizi. (alama 2)

Chakula chote kitaliwa. Chakula chochote kitaliwa.

(i) Weka nomino hizi katika ngeli mwafaka. (alama 3)

| Nomino | Ngeli |
|---|---|
| Maji | |
| Kipepeo | |
| Kulima | |

easytvet.com

(j) Bainisha silabi katika neno lifuatalo. (alama 2)

Nyweshwa

(k) Andika katika ukubwa wingi. (alama 2)

Njia hii inafaa kuliko ile.

## SEHEMU YA NNE: MBINU NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA (alama 20)

*Jibu mwaswali yote katika sehemu hii.*

4. (a) Wewe kama afisa anayeshughulikia maslahi ya jamii katika kaunti yako, umealikwa katika shule moja mashuhuri ili uwahutubie juu ya changamoto zinazowakumba vijana katika jamu na jinsi ya kukabiliana nazo. Eleza mbinu tano utakazotumia ili kufanikisha hotuba yako. (alama 10)

(b) Kumekuwa na mfululizo wa migomo ya mashirika mbalimbali katika nchi yetu. Wewe kama afisa wa uhusiano mwema, andika ushauri wa namna ya kukabiliana na tatizo hilo. (alama 10)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIYOPIGWA CHAPA.**

easytvet.com